TANGAZO LA SERIKALI NA. 1051 la tarehe 13/12/2025

SHERIA YA MISITU,

(SURA YA 323)

# NOTISI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 29)*

NOTISI YA KUSUDIO LA KUBADILI HADHI MSITU WA HIFADHI WA TAIFA NOU KUWA MSITU WA HIFADHI WA MAZINGIRA ASILIA NOU YA MWAKA 2024

KWA KUWA, eneo la Msitu wa Taifa Nou lilitangazwa chini ya Tangazo la Serikali Na. 94 la mwaka 1933 kuwa Eneo la Msitu wa Hifadhi wa Taifa Nou;

NA KWA KUWA, Waziri kwa mamlaka aliyopewa chini ya kifungu cha 29 cha Sheria ya Misitu, Sura ya 323 anaona kwamba ni kwa maslahi ya umma kubadili hadhi eneo la Msitu wa Hifadhi wa Taifa Nou kuwa Msitu wa Hifadhi wa Mazingira Asilia Nou; na

NA KWA KUWA, Waziri kwa kuzingatia Sheria ya Misitu, Sura ya 323 ambayo, pamoja na masharti mengine, inamtaka Waziri anapokusudia kubadili hadhi Msitu wa Hifadhi wa Taifa kuwa Msitu wa Hifadhi wa Taifa wa Mazingira Asilia kutoa Notisi ya kusudio kwa umma kabla ya kutekeleza mamlaka hayo;

HIVYO BASI, Waziri anatamka kama ifuatavyo:

Jina

1. Notisi hii itajulikana kama Notisi ya Kusudio la Kubadili Msitu wa Hifadhi wa Taifa Nou kuwa Msitu wa Hifadhi wa Mazingira Asilia Nou ya Mwaka 2024.

Eneo linalopendekezwa kutangazwa

2. Eneo la hifadhi lililo ndani ya mipaka iliyoainishwa katika Jedwali linapendekezwa kubadilishwa hadhi kuwa Msitu wa Hifadhi wa Mazingira Asilia Nou.

Madhumuni

3. Madhumuni ya kubadili hadhi ya Msitu wa

ya tangazo

Hifadhi wa Taifa Nou ni-

(a) kulinda eneo lililo hatarini la misitu ya nyanda za juu za kitropiki ambalo linatambulika kwa thamani yake ya juu ya baioanuwai, lenye upekee wa mimea na wanyama, ikijumuisha aina za mimea na wanyama walio hatarini, baadhi yao wako katika hatari ya kutoweka; na

(b) kulinda eneo la msitu na matumizi endelevu ya rasilimali za misitu katika eneo la msitu.

Uhalali wa Notisi

4.-(1) Notisi hii itakuwa halali kwa muda wa siku tisini kuanzia tarehe ya kuchapishwa katika Gazeti la Serikali.

(2) Ndani ya kipindi hicho cha siku tisini, mtu au kundi la watu au mwakilishi wao anaweza, kwa maandishi kuwasilisha pingamizi, maoni au madai ya haki yoyote inayotokana na sheria za kimila kuhusiana na ardhi au mazao ya msitu au haki yoyote iliyoainishwa kwenye sheria nyingine katika eneo ambalo linapendekezwa kubadilishwa hadhi kuwa Msitu wa Hifadhi wa Mazingira Asilia Nou.

Uwasilishaji wa pingamizi

5. Pingamizi, maoni au madai yoyote dhidi ya kusudio la kubadili hadhi ya Msitu wa Hifadhi wa Taifa Nou kuwa Msitu wa Hifadhi wa Mazingira Asilia Nou, yawasilishwe ndani ya siku tisini kuanzia tarehe ya kuchapishwa kwa Notisi hii kwa anuani ifuatayo:

Katibu Mkuu,
Wizara ya Maliasili na Utalii,
S.L.P. 1351,
DODOMA.

---

JEDWALI

---

*(Limetengenezwa chini ya aya* ya 2)


WILAYA YA MBULU NA BABATI

MSITU WA HIFADHI WA TAIFA WA MAZINGIRA ASILIA NOU

Makadirio ya eneo: Hekta 29812.232 au Kilometa za Mraba 298.12

Unakopatikana na Mipaka:

Eneo lote la hifadhi awali chini ya Eneo la Msitu wa Hifadhi wa Taifa Nou unaopatikana Wilaya ya Mbulu na Babati katika Mkoa wa Manyara kama lilivyochorwa upya katika Ramani ya Idara ya Upimaji Na. Jb 3082 (Skeli 1:50,000) iliyohifadhiwa na Mkurugenzi wa Upimaji na Ramani na lenye mipaka ifuatayo:




Dodoma
11Disemba, 2024

PINDI HAZARA CHANA
*Waziri wa Maliasili na Utalii*